HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

Simu: 026-2772614
Fax: 026-2772070
Email: ded@mufindi.go.tz
Web: www.mufindidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
S.L.P. 223,
Mafinga.

Mh. Mwenyekiti,
Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango

Hiki ni kikao cha kawaida cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha kujadili taarifa mbalimbali za Fedha, Uongozi na Mipango. Kikao hiki kinafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa na Memoranda ya Fedha ya Serikali za Mitaa agizo namba 21.Kwa msingi huo ni jukumu la kila mjumbe kupitia taarifa hii na kuchangia maoni ambayo yataisaidia Halmashauri kufikia lengo kuu la kutoa Huduma nzuri na endelevu zenye kuleta Maendeleo katika Wilaya yetu ya Mufindi.

- **Mapitio ya Bajeti 2017/18**

A) Mapato

Mh. Mwenyekiti,

Katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ilipitisha bajeti ya kukusanya na kupokea jumla ya Tshs.**51,837,410,700.05** Makusanyo haya yamegawanyika kama ifuatavyo;

Na.	Maelezo	Kiasi
1.	Mapato ya ndani	3,890,726,000.00
2.	Ruzuku Mishahara	34,456,072,480.00
3.	Ruzuku matumizi ya kawaida	2,985,977,000.00
4.	Ruzuku ya miradi ya maendeleo na Wadau wengineo	7,172,987,920.05
5	Nguvu za Wananchi	3,331,647,300.00
JUMLA		**51,837,410,700.05**

Aidha kwa mwaka wa fedha 2017/18, Halmashauri imeanza na bakaa yaTshs. **1,045,869,756.00** Fedha hizi zimegawanyika kama ifuatavyo;

Jina la akaunti	Namba ya akaunti	Kiasi
Matumizi ya kawaida	60210001175	13,576,535.08
Miradi ya Maendeleo	60210001176	590,915,991.91
Maji	60210004850	39,590,304.29
Mapato ya ndani	60210001172	183,421,565.51
Akaunti ya Mishahara	60210001174	114,890,860.00
Elimu	60210018989	195,880.31
Afya	60210018991	103,278,618.90
Jumla		**1,045,869,756.00**

Katika kipindi cha Julai – Septemba 2017 Halmashauri imepokea fedha nje ya makisio ya mwaka kiasi cha **Tshs 335,107,064.66**, Kati ya fedha hizo Kiasi cha **Tshs 276,617,850.10** ni kwa ajili ya Miradi ya TASAF na **Tshs 58,489,214.56** ni kwa ajili ya Mradi wa Bonde la Kihansi

Mh. Mwenyekiti,

Ukijumlisha fedha ya bakaa, makisio yaliyokuwa yameidhinishwa, bajeti ya Halmashauri kwa Mwaka 2017/2018 na Makisio ya nyongeza inakuwa na jumla ya Tshs.**53,218,387,490.71** kwa mchanganuo ufuatao;

Chanzo cha Mapato	Kiasi
Mapato ya ndani	4,047,724,070.59
Ruzuku ya Mishahara	34,570,963,340.00
Matumizi mengineyo	2,986,172,880.31
Nguvu za Wananchi	3,331,647,300.00
Miradi ya Maendeleo	8,241,879,899.81
Jumla	**53,218,387,490.71**

B) Matumizi

Mh. Mwenyekiti

Katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Halmashauri ya wilaya ya Mufindi inategemea kutumia jumla ya Tshs.**53,218,387,490.71** Matumizi hayo yamegawanyika kama ifuatavyo;

Chanzo cha Matumizi	Kiasi
Mishahara	34,589,425,340.00
Matumizi ya Kawaida	4,970,553,627.00
Miradi ya maendeleo	13,658,408,553.81
Jumla	**53,218,387,490.71**

2) Hali Halisi

A) Mapato

Mh. Mwenyekiti,

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2017, Halmashauri ilikusanya na kupokea jumla ya Tshs. **7,932,934,937.15**. Kati ya Mapato haya Tshs **561,375,182.59** ni mapato yaliyotokana na vyanzo vya ndani, Tshs **6,203,742,450** ni Mishahara, Tshs **836,560,704.56** ni Miradi ya maendeleo na Tshs **331,256,600.00** ni Matumizi ya kawaida.

Mlinganisho wa Mapato halisi ya Tshs **7,932,934,937.15** kwa kipindi cha Septemba 2017 na makisio ya Tshs **51,837,410,700.05** inaonesha kuwa Halmashauri imekusanya asilimia **16.33** ya lengo la mwaka wa fedha wa 2017/18.Aidha mlinganisho wa mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani yaliyokusanywa kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2017 ya Tshs**, 561,375,182.59** na Makisio ya mapato yanayotokana na vyanzo vya ndani ya Tshs **3,890,726,000.00** kwa kipindi hicho, yanaonesha kuwa Halmashauri imekusanya asilimia **14.43** ya lengo la mwaka .

Mh Mwenyekiti,

Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato katika kipindi cha Julai-Septemba 2017 unaonesha kuwa hali ya ukusanyaji wa mapato haikuwa ya kuridhisha . Hali hii inasababishwa na Msimu wa biashara ya mazao mbalimbali kuwa katika hali isiyokuwa yakuridhisha. Ushuru mwingi wa mbao hupatikana baada ya Sao Hill kugawa Plots. Aidha, Kwa upande wa chai kipindi hiki ni cha ukame na hivyo zao la chai linalovunwa ni kidogo.

Ili kukabiliana na hali hii Halmashauri imejipanga kufanya yafuatayo

- Kufanya doria kila siku ili kuwakamata wanaotorosha mbao bila kulipia
- Kila idara kusimamia chanzo chake cha mapato na kujiwekea mkakati wa kukifanya kianze kutumika ndani ya mwaka huu ikiwemo kupima viwanja Mwanzoni mwa robo ya kwanza ya 2017/18, kufuatilia uanzishwaji wa Stendi ya Nyololo
- Kusimamia matumizi ya Mfumo wa Ki Electronic wa ukusanyaji wa mapato kwa kuongeza machine za kukusanyia mapato ili kila Sehemu yenye mapato ya kutosha kupatiwa machine hizo
- Kuendelea kuwatambua Wafanyabiashara wanaofanya biashara katika Eneo la mamlaka ya Halmashauri ya wilaya ya Mufindi ili waweze kulipa kodi na Leseni za Biashara
- Kuendelea kulipa 25% kwa vijiji na kata ili kuongeza morale ya ukusanyaji wa mapato

B) Matumizi

Mh. Mwenyekiti,

Matumizi hutegemea mapato yanayokusanywa. Kwa kipindi Septemba 2017, Halmashauri imetumia kiasi cha **Sh. 7,507,026,804.54** hadi kufikia 30/9/2017. Matumizi hayo yamegawanyika kama ifuatavyo,

Chanzo cha Matumizi	Kiasi
Mishahara	6,203,744,449.99
Matumizi mengineyo	404,805,910.08
Miradi ya maendeleo	898,476,444.47
Jumla	**7,507,026,804.54**

3) Taarifa Nyinginezo

a) Usuluhisho wa Benki

Mh. Mwenyekiti,

Usuluhisho wa benki kwa mwezi Septemba 2017 umefanyika kwa akaunti zote tisa kama ifuatavyo,

Na	Jina la Akaunti	Salio Benki	Salio la Kwenye Vitabu
1	Miradi ya Maendeleo (60210001176)	1,090,106,133.03	734,995,879.78
2	Mishahara (60210001174)	115,725,588.20	115,725,588.20
3	Mradi wa Maji (60210004850)	38,387,104.29	34,337,104.29
4	Afya (60210018991)	55,143,503.94	73,400,245.94
5	Elimu (60210018989)	3,740,655.91	3,740,655.91
6	Other Charges (60210001175)	105,038,983.02	45,930,866.67
7	Deposit (60210001177)	468,316,810.36	436,517,510.36
8	Own Source (60210001172)	51,627,029.58	51,627,029.58

b) Akaunti ya Amana

Akaunti ya Amana huweka amana mbalimbali. Wakati tunaanza mwaka huu wa fedha (1/7/2017) mfuko huu ulianza na salio anzia la Tshs. **153,932,076.57** Mapato kwa mwezi Julai - Septemba 2017 yalikuwa Tshs **446,518,313.70** na hivyo kuifanya Akaunti hii kuwa na jumla ya Tshs **600,450,390.27** ilipofika tarehe 30/9/2017. Aidha Matumizi kwa Mwezi Julai – Septemba 2017 ni Kiasi cha Tshs **163,932,879.91** na hivyo kufanya Akaunti hii kuwa na bakaa ya Tshs **436,517,510.36**

c) Madeni

Mh. Mwenyekiti,

c) Madeni

Mh. Mwenyekiti,

Wakati tunaanza mwaka huu wa Fedha (2017/18), Halmashauri ilikuwa na deni ya Tshs.**570,907,693.76**. Hadi tarehe 30/9/2017 jumla ya deni lenye thamani ya **Tshs 17,564,084.25** lilikuwa limelipwa na hivyo Halmashauri kubakia na deni la **Tshs 553,343,609.51**

Mh. Mwenyekiti,

Pamoja na Taarifa hii nimefungasha Jedwali Mbalimbali zinazoonesha mwenendo wa mapato na matumizi katika kipindi hiki

Mh. Mwenyekiti,

Naomba Kuwasilisha.

Felisi B. Mhando
KNY: MKURUGENZI MTENDAJI WILAYA
MUFINDI